

HALMASHAURI YA MANISPAA SUMBAWANGA

Tel: +25 25 -2802163

Fax: +255 25 2802163

E-mail: md.sumbawanga@rukwa.go.tz



P.O. Box 187
SUMBAWANGA

06/04/2017

TAARIFA KWA UMMA

Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga inatarajia kuupokea Mwenge wa uhuru ukitokea Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo tarehe 9, Aprili, 2017 saa mbili asubuhi katika kijiji cha Tamasenga, Kata ya Pito.

Mbio za mwenge zinatarajiwa kuzindua ama kuweka jiwe la Msingi katika miradi isiyopungua 13 yenye thamani ya shilingi 8,253,569,993. Na kutembelea vikundi 10 vya kuhamasisha upingaji wa Rushwa, Madawa ya Kulevya na kupunguza maambukizi ya UKIMWI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga anawaomba wananchi wote kujitokeza katika Maeneo ya miradi ambayo Mwenge wa Uhuru utapita ili kuusheherekea na kuunga mkono kauli mbiu ya mwaka huu isemayo, **“Shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya Nchi.”**

Pamoja na kauli mbiu hii mbio za Mwenge wa uhuru zitaendelea kuihamasisha jamii ya Watanzania kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa, mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, Mapambano dhidi ya matumizi ya Dawa za Kulevya na mapambano dhidi ya Malaria.

Pamoja na hayo usiku wa tarehe 9, Aprili 2017 Mwenge wa Uhuru unatarajiwa kukesha katika viwanja vya shule ya Msingi Ndua, vilivyopo kata ya Kizwite. Wananchio wote tunaomba kujitokeza kwa wingi.

Abdulrahman Salim Ally

Afisa Habari

Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

06, Aprili, 2017.